




Viwango vya Kilimohai Afrika Mashariki

Ufugaji wa Nyuki




**Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania- TOAM,
2026**



In cooperation with



- Ni mfumo wa ufugaji nyuki unaozingatia afya ya nyuki, mazingira ya kiasili, na kuepuka matumizi ya kemikali kwa lengo la kuzalisha asali na bidhaa nyingine zisizo na mabaki ya kemikali.
- Ufugaji nyuki huchangia kuongeza uzalishaji wa kilimo na misitu kupitia uchavushaji wa mazao unaofanywa na nyuki.



Ufugaji nyuki wa kilimohai husaidia:

- Kulinda mazingira
- Kuboresha uchavushaji wa mazao
- Kuzalisha asali bora
- Kulinda afya ya nyuki
- Kupunguza matumizi ya kemikali



Mahitaji ya jumla

Mahali pa Mzinga wa Nyuki: EAOPS sehemu ya 8.2.2

- Weka mizinga mbali na maeneo yenye uchafuzi kama mashamba yanayotumia kemikali, viwanda, dampo, barabara na maeneo yenye uchafuzi mkubwa angalau kilomita 5
- Hakikisha nyuki wanapata chavua nanekta kutoka kwenye mimea ya asili au ya kilimohai ndani ya kilomita 3 kuzunguka mzinga.
- Hakikisha mazingira yanayozunguka mizinga yana mimea ya kutosha kwa nyuki kupata chakula mwaka mzima.



Vifaa vya Mzinga: EAOPS Sehemu ya 8.2.3

- Mizinga itengenezwe zaidi kwa vifaa vya asili visivyoweza kuchafua mazingira au bidhaa za nyuki.
- Matumizi ya vifaa vyenye sumu au kemikali hatarishi hayaruhusiwi.
- Usitumie vifaa vya mzinga vinavyoweza kuacha mabaki ya kemikali kwenye asili au nta



Kulisha nyuki: EAOPS sehemu ya 8.2.4

- Mwisho wa msimu, hakikisha mzinga una akiba ya kutosha na asali na chavua kutosha ili nyuki waweze kujitegemea.
- Ikiwa chakula cha ziada kinahitajika tumia asali ya kilimohai au sharubati ya sukari ya kilimohai

Kubadilisha kwenda ufugaji nyuki wa kilimohai : EAOPS sehemu ya 8.2.5

- Makoloni ya nyuki yanaweza kubadilishwa kwenda mfumo wa kilimohai.
- Nyuki wapya watoke kwenye vyanzo vya kilimohai inapowezekana.
- Wakati wa kipindi cha mpito, nta ya zamani ibadilishwe na nta ya kilimohai.



- Ikiwa nta yote ya zamani haijaondolewa ndani ya mwaka mmoja, kipindi cha mpito kitaongezwa hadi nta yote ibadilishwe.
- Asali inaweza kuuzwa kama ya kilimohai baada ya angalau msimu mmoja kamili wa usimamizi wa kilimohai.

Afya ya Nyuki na Udhibiti wa Magonjwa: EAOPS sehemu ya 8.2.7

- Dumisha afya ya mzinga kwa kutumia usafi mzuri na usimamizi wa mara kwa mara wa mzinga.
- Tumia kwanza tiba za asili kudhibiti magonjwa.
- Tumia njia za asili kama tindikali za asili, mafuta tiba ya asili, na mvuke au moto kwa usafishaji.
- Ikiwa mzinga umetibiwa kwa dawa za kemikali, utenganishwe na mizinga ya kilimohai na upitie kipindi cha mpito cha mwaka mmoja kabla ya kurudi kwenye uzalishaji wa kilimohai.
- Ondoa kizazi cha dume pale tu inapohitajika kudhibiti wadudu wa varroa.
- Mafuta ya injini yalitoyumika hayapaswi kutumika kama njia ya kudhibiti wadudu.
- Upandikizaji wa mbegu kwa njia ya bandia kwa malkia nyuki unaruhusiwa.
- Wakati wa uvunaji na uchakataji, hakikisha joto la asali halizidi 45°C ili kuhifadhi ubora wake wa asili na virutubisho vyake



HAIRUHUSIWI:

- Kuua nyuki wakati wa uvunaji
- Kukata mabawa ya malkia wa nyuki
- Kutumia kemikali kufukuza nyuki au vifaa vinavyoweza kuchafua asali au nta.
- Matumizi ya moshi wakati wa uvunaji yapunguzwe kadri iwezekanavyo.

Kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki kinaonesha mahitaji ya msingi ya viwango vya bidhaa za kilimohai vya Afrika Mashariki vijulikanavyo kama East Africa Organic Products Standards (EAOPS). Kiwango hiki kilipitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 na kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka mitano hivyo kuwa kiwango rasmi kwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Kipeperushi hiki rahisi kimeandaliwa na Mwamvuli wa Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement -TOAM) kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya Kilimo Ikolojia Hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology in East Africa – KHEA).

Mradi huu unalenga kuandaa, usambazaji wa maarifa na matumizi ya kilimo Ikolojia hai katika Afrika Mashariki. Unafadhiliwa na GIZ kupitia Biovision African Trust (BvAT)

Unaweza kupata maarifa kama haya na mengine mengi kutoka Tanzania na afrika kwa ujumla kwa kutembelea tovuti: <https://khea-africa.org/> na <https://kcoa-africa.org/>
KHEA Website

Mawasiliano

 info@kilimohai.org

 +255 744 134 999

Machapisho mengine katika mfululizo huu

- Uzalishaji wa mazao
- Uzalishaji wa Mifugo
- Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai
- Uzalishaji wa Viumbe Maji